

Maswali

1. Abramam aliishi wapi na kulikuwaje?
2. Watu wa Uru waliabudu nini?
3. Abramam alifanya nini alipoambiwa na Mungu aiache nyumba yake, jamaa na marafiki?
4. Abramam alienda na nani?
5. Abramam alisimama wapi njiani?
6. Mungu aliwapeleka nchi gani?
7. Abramam alijenga nini kama shukurani kwa Mungu?
8. Ahadi zipi 3 Mungu aliahidi Abramam?
9. Nani mzao wa maana (pekee) wa Abramam?
10. Ni wakati gani atafurahisha watu wote?

Majibu


1. Abramam aliishi mji wa Uru na ulikuwa mji wa waovu.
2. Watu wa Uru waliabudu mwezi.
3. Abramam aliacha nyumba yake, jamaa na marafiki na akaenda mji mwingine.
4. Alienda na Sarai na Lutu.
5. Njiani, Abramam alisimama Harani.
6. Mungu aliwapeleka nchi ya kanaani.
7. Abramam alijengea Mungu madhabu.
8. Mungu aliahidi kwamba Abramam atakuwa:
 - Na wazao wengi
 - Mashuhuri na sifa njema
 - Na mzao wa pekee maalum atakayefurahisha kila mtu duniani.
9. Yesu.
10. Yesu atafurahisha kila mtu katika ufalme.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

5 Kuitwa kwa Abramam



Marejeo

Mwanzo 12 – 13

Kiini cha somo

Kuonyesha vile Mungu aliahidi Abramam ahadi maalum na vile Abramam alizitii. Tena kuonyesha vile hizi ahadi zitalindwa.

Maneno maalum

1. Uru + Mji muovu + Mwezi
2. Abramam + tawi + nchi geni + Baraka
3. Alitii Mungu + Sarai na Lutu + hema
4. Safari + Harani
5. Kanaani + shukuru Mungu.
6. Ahadi + Yesu atatimiza hizo ahadi za Mungu kwa Abramam

5.1 Karibu na Mto Frati ulikuwepo mji ulioitwa Uru. Uru ulikuwa mji mkubwa zaidi ya miji katika nchi hiyo.

Mtu aliyeitwa Abram u aliishi katika mji wa Uru yeye na jamaa yake. Nao walikuwa matajiri pia waliishi katika majumba makubwa. Labda walikuwa na watumwa wengi. Watu waliokuwa wakiishi Uru waliabudu mungu potovu mwezi, ila Abram alimpenda Mungu wa kweli aliyemwabudu.

5.2 Siku moja Mungu alimwambia Abram, "Nakutaka utoke katika mji huu. Ondoka Uru na uiache nyumba yako na jamaa na rafiki zako. Utatembea mwendo mrefu hadi nchi iliyo mbali. Nitakuonyesha njia ya kwenda. Kama ukinitii nitakubariki."

Mungu alitaka kuona iwapo Abram alimpenda zaidi kuliko utajiri wake wote na jamaa yake na rafiki zake. Mungu alitaka kujua ikiwa Abram atamtumainia vya kutosha kiasi cha kuiacha nyumba yake na kufuata njia ambayo Mungu atamwonyesha.

Mungu alimchagua katika watoto wote maelfu wa Nuhu. Mungu alimchagua Abram kwa kuwa alikuwa mtu mwenye haki na mwaminifu. Mungu alimchagua Abram kuwa baba wa watu mahususi wa Mungu. Mungu alitoa ahadi maalum kwa Abram.

5.3 Upendo wa Abram kwa Mungu ulikuwa mkubwa sana. Alifanya kile ambacho Mungu alimtaka afanye. Abram aliondoka Uru akiwa na baba yake, mkewe na binamu yake, Lutu. Waliondoka mji wa Uru wakasafiri kuelekea kaskazini. Abram alimpenda sana Mungu kabisa na alimtii. Aliondoka nyumbani kwenye kila kitu akawaacha rafiki zake wote. Abram alisafiri mwendo mrefu sana. Alikaa katika hema akaenda kuishi nchi ngeni mahali ambako hakuwa na rafiki. Abram hakutaka lolote zaidi kuliko kumpendeza Mungu na kuishi katika Ufalme wake.

5.4 Abram akasafiri kuelekea kaskazini toka mji wa Uru. Baba ya Abram alikuwa mzee sana. Alichoka sana kusafiri kila siku. Abram alipofika mji wa Harani, alikaa pale kwa muda. Baada ya muda fulani baba yake Abram akafariki wakiwa katika mji wa Harani.

5.5 Baada ya kufa baba yake Abram, Abram, Sarai na Lutu wakaondoka tena hapo. Mungu aliwaonyesha njia ya kwenda. Hatimaye wakafika katika nchi ya Kanaani. Hiyo ndiyo nchi alivyowaleta Mungu. Abram akajenga madhabahu na kutoa sadaka ya kumshukuru Mungu. Alimshukuru Mungu kwa kumleta salama katika nchi hii ngeni.

5.6 Mungu alipendezwa sana kwa kuwa Abram alimpenda na kumtii. Mungu alifurahi sana kwa kuwa Abram alimtumainia na kuziamini ahadi zake. Mungu akambariki Abram na kufanya ahadi muhimu sana kwake

5.7 Ahadi za Mungu kwa Abram

- Abram atakuwa na watoto wengi. Watakuwa na taifa kubwa. Watoto wa Abram, Wayahudi, sasa wamekuwa ni taifa kubwa.
- Abram atakuwa mtu mashuhuri na kuwa baraka kwa ulimwengu uliobaki. Hata sasa tunajifunza habari za Abram, hivyo amekuwa maarufu.
- Watakuwa watu maalum kwa Mungu, kwa hiyo hao wenye anawabariki hubarikiwa na wenye kuwalaani hulaaniwa. Mungu aliwatumia Waisraeli wakiwa ni watu wake maalum, ili kutupa neno lake, Biblia.
- Kwa njia ya watoto wa Abram watu wa dunia watapata furaha. Huyo mtoto pekee wa Abram ni Yesu Kristo.

